

COVID-19 attendance advice for families

| Idara ya Elimu ya NSW

Ushauri wa kuhudhuria kwa COVID-19 kwa familia

[Idara ya Afya ya NSW](#) ilitoa ushauri mpya wa COVID-19 kwa shule tarehe 14 Agosti 2020. Huu unabadilisha jinsi shule zetu zinavyofanya kazi.

Watoto ambao ni wagonjwa wenye dalili kama za homa ya mafua, hata ikiwa ni dalili kidogo, wanapaswa kukaa nyumbani. Watoto ambao wanakuwa wagonjwa shuleni watakaa kwenye chumba cha wagonjwa na mipango itafanywa ili watachukuliwa.

- Idara ya Afya ya NSW imeomba kuwa shule zitie moyo mtu yeyote ambaye hajisikii vizuri au ana dalili kidogo kama za homa ya mafua, kupanga kupimwa kupitia mtaalamu wao wa matibabu au mojawapo ya [zahanati ya COVID-19](#).
- Wanafunzi na wafanyakazi walio na dalili kama za homa ya mafua watahitaji kutoa nakala ya matokeo ya kipimo cha COVID-19 yanayoonyesha hana kabla ya kuruhusiwa kurudi shuleni.

Huduma ya Ukalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji habari zaidi tafadhali piga simu kwa mwalimu mkuu wa shule yako. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia kwa maswali yako tafadhali piga simu kwa Huduma ya Ukalimani wa Simu kwenye 131 450 na uombe mkalimani kwa lugha yako. Huduma hii itakuwa ya bure kwako.